# Jarida la KILIMO

**Toleo la Tano**
**Januari - Machi, 2011**




*Mhe: Balozi Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Raisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiweka jiwe la msingi katika jengo la Kituo cha Mafunzo ya Usarifu wa Mazao kilichopo Kizimbani*

## Yaliyomo

Maoni ya Mhariri/ Picha ya Jalada....................Uk.2
Tathmini ya athari ya jua kali katika mabonde ya mpunga....................Uk.3
Ziara ya Makamo wa Kwanza wa Rais katika Wizara ya Kilimo....................Uk.4 - 5
Ugawaji wa mbegu ya msaada kwa wakulima walioathirika na jua....................Uk.6
Malighafi kwa ajili ya kusarifu....................Uk.7
Matukio katika Picha....................Uk.8 - 9
Warsha ya Sera ya Uhakika wa chakula kwa Wawakilishi....................Uk.10
Umuhimu wa zao la karoti....................Uk.11
Uvumbikaji na Ukaushaji wa vanila....................12
Utunzaji wa vifanga vya kuku....................Uk.13
Udhibiti wa wadudu waharibifu wa minazi....................Uk.14
Uvunaji wa maji ya mvua....................Uk. 15
Mradi wa kukuza mashirikiano ya nchi za bahari ya Hindi....................Uk.16

## Bodi ya Wahariri

Mshauri
Affan O. Maalim

Mhariri Mkuu
Dk. Juma M. Akil

Msanifu na Mhariri Mtendaji
Hashim H. Chande

Wahariri Wasaidizi

Makame M. Abdulrahman

Nassor S. Mkarafuu

Othman A. Maulid

Nassor S. Mohammed

Mpiga chapa
Tamasha M. Suleiman

Mpiga picha
Khamis A. Bakari

ANUWANI
Wizara ya Kilimo,
Maliasili - Zanzibar
S.L.P. 159
Simu: +255 24 2230986
Fax: +255 24 2234650
E-mail: kilimo@zanlink.com
Tovuti: kilimoznz.or.tz

# MAONI YA MHARIRI

Ndugu Wakulima; sote tunakubaliana kwamba kilimo cha umwagiliaji maji ndio mkombozi wetu kwa ukulima wa mpunga, umuhimu wake umezidi kuwa mkubwa kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa yanayotokea duniani kote, hali inayosababisha kilimo cha kutegemea mvua kutokuwa cha uhakika na cha matumaini. Hivyo, tunahitaji kujipanga vyema na kukiimarisha kilimo cha umwagiliaji maji ili tuwe na uhakika wa chakula na kupunguza uagizaji.

Kwa mujibu wa Mpango Mkuu wa Umwagiliaji maji wa mwaka 2003, Zanzibar tunalo eneo la ekari 21,300 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji. Hadi sasa eneo lililojengwa miundombinu ni ekari 1,750 sawa na asilimia 8% tu ya eneo lote. Eneo lililobaki lenye ukubwa wa ekari 19,550 kati ya hizo ekari 200 zimejengwa makinga maji, ekari zilizobaki 19,350 zinaendelea kutumika kwa uzalishaji wa mpunga wa kutegemea mvua.

Ndugu Wakulima pamoja na hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa miundombinu, bado tunakabiliwa na changamoto za gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu, ukarabati wa visima na pampu kutokana na teknolojia duni upungufu wa wataalamu na elimu ya uendeshaji wa jumuiya za wakulima na upungufu mkubwa wa mitaji, utegemezi mkubwa wa nishati ya umeme, uharibifu wa vianzio vya maji pamoja na ukosefu wa zana maalum za utayarishaji wa ardhi. Kutokana na changamoto hizo hadi sasa zaidi ya asilimia 90 ya eneo linalofaa kwa umwagiliaji maji linalimwa kwa kutegemea mvua hali ambayo inapelekea uzalishaji na tija ndogo.

Ndugu Wakulima, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo 2011 – 2016 Wizara ya Kilimo na Maliasili imekusudia kuutekeleza kikamilifu Mpango Mkuu wa Umwagiliaji maji ambao unatarajiwa kutatua changamoto zote za kilimo hicho. Wizara imezungumza na Serikali ya Korea kupitia Benki ya EXIM – ambao wamekamilisha uhakiki wa eneo la ekari 5250 ambalo litajengwa mindombinu ya umwagiliaji maji. Serikali ya Japan na Benki ya BADEA pia wameonesha nia ya kutusaidia katika Kilimo cha umwagiliaji maji.

Ndugu Wakulima, Wizara imekusudia kuendeleza ujenzi wa miundombinu na utunzaji wa vianzio vya maji ili sekta ya umwagiliaji maji ipate maendeleo endelevu na kuwawezesha wakulima kuongeza tija na uzalishaji wa zao la mpunga. Kuzijengea uwezo Jumuiya za Wakulima wa umwagiliaji maji ziweze kushiriki kikamilifu katika uendeshaji na utunzaji wa miundombinu, uhifadhi wa vianzio vya maji na utoaji wa huduma za Kilimo. Wizara inaendelea kuwashajihisha wananchi kushiriki kikamilifu katika kuchagua miradi ya kijamii ya umwagiliaji maji ikiwemo ujenzi wa miundombinu na makinga maji kila wanapopata fursa ya usaidizi wa Washirika wa Maendeleo.

Ndugu Wakulima, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wakulima wa mpunga wa umwagiliaji maji watumie mbegu bora na pembejeo zinazotolewa na Wizara ya Kilimo na Maliasili ili kuongeza tija na uzalishaji wa zao hilo na kuhakikisha kuwa miundombinu ya umwagiliaji maji iliyojengwa kwa gharama kubwa tunaitumia kikamilifu katika uzaalishaji wa zao hili.

# PICHA YA JALADA

Katika picha anaonekana Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi akiweka jiwe la msingi katika kituo cha mafunzo ya Usarifu wa Mazao kiliopo katika kituo cha kilimo, Kizimbani kinachojengwa kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA) katika kuadhimisha miaka 47 ya Mapinduzi ya Zanzibar, tarehe 7 Januari 2011.

# TATHMINI YA ATHARI ZA KIANGAZI KATIKA MABONDE YA MPUNGA

Na Othman A. Maulid

Mnamo tarehe 21 hadi 26 Febuari, 2011 Wizara ya Kilimo na Maliasili ilifanya tathmini ya athari iliyojitokeza katika baadhi ya maeneo ya mabonde yanayolimwa mpunga Unguja baada ya mazao mengi kuathirika kutokana na kiangazi. Tathmini hiyo ilihusisha mabonde ya Kijitoupele, Kwarara, Kizimbani, Mfenesini na Kama kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi, mabonde ya Koani, Kisima mchanga, Kiboje, Miwani, Mchangani, Cheju, Muyuni na Mtende kwa Mkoa wa Kusini na mabonde ya Kilombero, Kibokwa, Jangwani na Kibonongwa kwa Mkoa wa Kaskazini.

Kutokana na athari hiyo Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi alifanya ziara maalum kuyatembelea mabonde ya mpunga ulioathiriwa na jua kali katika Mkoa wa Kaskazini na kuangalia hali halisi ya athari hiyo.



Mhe. Balozi Seif Ali Iddi Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar wa pili kushoto, Mhe. Mansoor Yussuf Himid Waziri wa Kilimo na Maliasili wa kwanza kulia pamoja na ndugu Affan Othman Maalim Katibu Mkuu wa Wizara hiyo wa kwanza kushoto wakiangalia mpunga uliokauka kutokana na kiangazi katika bonde la mpunga la Kilombero

## MAENEO YALIYOFANYIWA TATHMINI NA HALI ILIVYOKUA

Mkoa wa Kusini Unguja ekari zote zlizopandwa mpunga ni 2,974 ambapo Wilaya ya Kati zilikuwa ekari 2,893 na Wilaya ya Kusini ekari 82 Jumla ya ekari 1,118 ziliathirika na kiangazi sawa na asilimia 39. Athari hiyo haikuwa kubwa na mpunga haukufikia kiwango cha kufa kabisa katika mabonde ya Cheju, Muyuni na Mtende kutokana na kupata mvua za awali jambo ambalo lilisaidia mpunga mwingi kuchipua vizuri. Katika mabonde ya Koani, Kisima mchanaga, Kiboje, Miwani na Mchangani hali ilikua mbaya sana kwani baadhi ya mpunga uliochipua ulikauka kwa jua na hakukua na matarajio ya kuota tena.

Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini jumla ya ekari 3,601 zilipandwa mpunga kati ya hizo ekari 1,669 zilizoathirika sawa na asilimia 46. Katika mabonde ya Kilombero, Kibokwa, Jangwani, Kibonongwa hali ya uotaji wa mpunga haikua nzuri kwa baadhi ya maeneo kwani yalipata mvua kidogo iliyosababisha kuoza kwa mbegu.

Nako katika Mkoa wa Mjini Magharibi jumla ya ekari 210 zilipandwa mpunga, ekari 158 ziliathirika sawa na asilimia 75. Mabonde ya Kijitoupele, Kwarara, Kizimbani, Mfenesini na Kama hali ya uotaji wa mpunga haikua nzuri na mpunga mwingi imeharibika.

## ATHARI KWA UJUMLA KATIKA MABONDE YOTE YA UNGUJA

Jumla ya ekari 5,640 zilipandwa mpunga katika kisiwa cha Unguja, kati ya hizo ekari 3,945 ziliathirika sawa na asilimia 70

# ZIARA YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS WA ZANZIBAR KATIKA MAENEO YA KILIMO NA MALIASILI

Na Hashim H. Chande

Mnamo tarehe 25 hadi 27/01/2011, Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Seif Sharif Hamad, akiongozana na wenyeji wake Mhe. Mansoor Yussuf Himid, Waziri wa Kilimo na Maliasili, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu na watendaji wa Wizara, alifanya ziara ya kuitembelea maeneo ya Kilimo na Maliasili.



Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Seif Sharif Hamad wa kwanza kushoto akiangalia ramani ya msitu wa Masingini na kupata maelezo kuhusu msitu huo kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu wa Maliasili, ndugu Bakar S. Aseid wapili kulia.

Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa kazi za kilimo na maliasili. Kabla ya kuanza ziara Mhe. Seif Sharif alionana na kuzungumaza na watendaji wakuu wa Wizara hiyo na vitengo vyake na kupokea taarifa za utekelezaji, mafanikio na changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo na maliasili. Mhe. Seif Sharifu alitembelea baadhi ya maeneo yanayosimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili, wakulima na wafugaji katika maeneo yao na kujionea miradi wanayoitekeleza.

Katika ziara yake hiyo ya siku tatu Mhe. Seif Sharif altembelea na kuzungumza na watendaji na wakulima katika maeneo yafuatayo:

Hifadhi ya msitu wa Masingini ambao ni chanzo kikuu cha maji yanayotumiwa na asilimia 80 ya wakaazi wa mji wa Zanzibar, msitu ambao kwa sasa unakabiliwa na changamoto kubwa ya uharibifu hasa kutokana na mahitaji ya ujenzi, makaazi na nishati,

Kituo cha uzalizashaji miche ya minazi Kidichi ambacho ni tegemeo kubwa la Serikali katika kutoa miche na taaluma bora za upandaji wa zao hilo,

Kituo cha Utafiti wa Kilimo Kizimbani ambacho hufanya tafiti za mbegu bora na maradhi ya mimea na kujionea tafiti za mbegu bora za mpunga wa juu aina ya NERICA, maabara za utafiti wa udongo,utafiti wa wadudu waharibifu na udhibiti wa nzi wa embe, Kituo cha Mafunzo ya Usarifu wa mazao, chuo cha kilimo, mashamba ya utafiti wa mazao ya mizizi na viungo.

Kituo cha upashanaji habari wakulima na mradi wa jamii wa duka la pembejeo Dunga na kituo cha uzalishaji wa mbegu za nafaka Bambi.

Bonde la uzalishaji mpunga Cheju ambapo alizindua upandaji wa mpunga wa kutegemea mvua kwa msimu wa mwaka 2011/2012, na Shamba la misitu la Serikali Kibele.

Hifadhi ya Taifa ya Msitu wa Jozani ambao ni kivutio kikubwa kwa watalii na kutokana na kuwa na misitu na viumbe ambavyo havipatikani duniani kote isipokuwa Zanzibar.

Kikundi cha wafugaji wa nyuki Kitogani na mkulima kijana wa migomba wa Kajengwa ambae amefanikiwa kutokana na kuiga taaluma kutoka kwa wakulima wenzake.

Ziara ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilikamilika kwa kutembelea kituo cha uimarishaji miche ya misitu Mwanyanya kuangalia kazi za uzalishaji miche na mto uliokauka kutokana na uharibifu wa misitu na ujenzi holela pembezoni mwa kituo hicho, mto ambao ulikuwa ukitumiwa na kituo kwa kazi za umwagiliaji maji vitaluni.

Bonde la mpunga wa umwagiliaji maji Kibokwa, wakulima wa mboga mboga wa bonde la mpunga Machekechuni ambalo hulitumia kwa kilimo cha mboga mboga baada ya mavuno ya mpunga, mfugaji kijana mzoefu wa kuku na mabata katika kijiji cha Kandwi, Mkoa wa Kaskazini – Unguja, shamba la misitu Chaani Masingini, shamba la uzalishaji wa maua liliopo Upenja ambalo linalomilikiwa na mwekezaji kutoka nchini Uholanzi, mradi wa jamii wa ufugaji wa mbuzi wa maziwa Tazari na kumtembelea muwekezaji mzalendo wa zao la embe katika kijiji cha Fuoni Kibondeni.

Mhe. Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais, katika ziara yake hiyoaliipongeza Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa juhudu yake za kuendeleza kilimo na maliasili na kufanya kazi zake kwa ufanisi. Aidha, aliufurahishwa na juhudi za Wizara za kuanzisha vituo vya upashanaji habari na mabaraza ya wakulima katika kila wilaya ili kusaidia juhudi zake za uenezaji wa habari na taaluma za kilimo, ufugaji, maliasili na utafiti miongoni mwa wakulima na wafugaji.

Mhe. Seif Sharif Hamad alifurahishwa na vijana waliowekeza katika kilimo na ufugaji, akiwemo alieekeza katika kilimo cha Migomba, Makunduchi na

aliyeekeza katika ufugaji wa kuku na mabata huko Kandwi. Pia aliwataka vijana na wananchi wengine kuiga mafanikio na juhudi za vijana hao ili waweze kujiajiri, kuongeza kipato na kutoa mchango mkubwa katika sekta ya kilimo, ufugaji na maliasili, kazi ambayo itawawezesha kuibadilisha nchi yetu kujitosheleza kwa chakula na kupata tija badala ya kuutumia muda ambao ungelitumika kwa kazi za uzalishaji kukaa barazani kuzungumza, kucheza karata, kuzurura ovyo, kutumia madawa ya kulevya na kuwataka kuacha dhana kuwa kilimo ni kazi ngumu na haina tija. Aidha, aliwapongeza wanajamii wa Tazari kwa juhudi zao kundeleza ufugaji wa mbuzi wa maziwa na kuwataka kuendelea kuongeza uzalishaji wa maziwa na mbuzi ili kujiongezea kipato na kuziendeleza familia zao.

Mhe. Seif Sharif alifurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na mfugaji wa nyuki wadogo wa Kitogani kwa kuwafuga na kuwazalisha nyuki ambao wako hatarini kutoweka. Katika kuunga mkono juhudi hizo aliahidi kuchangia mizinga 10 ya kufugia nyuki hao ambapo wizara ya kilimo imeahidi kuchangia mizinga mitano.

Mhe. Seif Sharif alifurahishwa na uwekezaji wa shamba la maua la Kiwengwa na kusema kuwa huu ni ushahidi tosha kuwa Zanzibar inaweza kuzalisha maua yenye thamani kubwa ambayo yanastawi katika nchi za baridi ikiwa miundombinu mizuri ya uzalishaji itawekwa, kuchangia katika pato la pesa za kigeni na kuondoa dhana kwamba maua hayo yanaota katika maeneo yenye baridi tu kama vile Kilimanjaro na Arusha kwa Tanzania na Nairobi kwa Kenya. Vile vile alifurahishwa na mwekezaji wa zao la embe na kuwataka wananchi wengine wajitokeze kwa wingi kuwekeza katika kilimo na misitu ili kujipatia fedha za kigeni, kujikimu kimaisha na kuipatia Serikali mapato, badala ya kuwekeza katika biashara nyengine kama vile vituo vya mafuta.



Mhe. Seif Sharif Hamad akipata maelezo ya ufugaji bora wa mbuzi wa maziwa kutoka kwa mfugaji huko Tazari wakati wa ziara yake.

Mhe aliwapongeza wanaushirika wa duka la pembejeo Dunga Bweni kwa ufanisi wao na kuwasisitiza kuendelea na utunzaji wao mzuri wa mali za kikundi kwa kuhakikisha wanaowapa dhamana na majukumu ya kutunza mahesabu ni waaminifu na wanafuata taratibu za kufunga mahesabu na kuweka kumbukumbu ili kuepuka uganganyifu na upotevu wa mali za kikundi. Aidha, aliwataka wakulima wa bonde la mpunga la Cheju kuyatumia vizuri maeneo yote ambayo yanaweza kuzalisha mpunga na kuzalisha kwa wingi kwa vile mchele ndio chakula kinachotumika na kupendwa sana na wazanzibari na alisitiza kuacha kutegemea kuagiza kutoka nje ya nchi kutokana na kupanda kwa bei za vyakula duniani hasa nafaka.

Mhe. Seif Sharif alisikitishwa uharibifu wa mazingira ikiwemo ukataji wa miti na uharibifu wa vyanzo vya maji ambapo alikemea vikali tabia hiyo na kuagiza kusitishwa mara moja tabia hiyo na kuikamatwa kwa misumeno ya moto inayotumika kukata misitu ili kudhibiti athari hizo.

Aidha, alisikitisha na athari ya kiangazi kilichosababisha kukauka kwa mito inayotegemewa kwa kumwagilia maji katika bonde la Machekechuni kuliko sababisha kuwakosesha wakulima wa hapo kipato kitokanacho na kuuza mboga mboga Katika kukabiliana na hali hiyo aliahidi kusaidia fedha za kuchimbia kisima kwa ajili ya kumwagilia maji mboga mboga.



Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mhe. Seif Sharif Hamad wa kwanza kushoto akiwa na mwenyeji wake Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid kati kati akiangalia mbegu za mpunga na katika kituo cha Utafiti Kizimbani na kupata maelezo kuhusu tafiti hizo kutoka kwa mtafiti ndugu Khatib Juma.

# WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI YAKABIDHI MSAADA WA MBEGU YA MPUNGA KWA WAKULIMA

Na Othman A. Maulid

Kufuatia athari iliyotokana na jua kali iliyoyakumba mabonde ya mpuga katika msimu huu na kuathiri mbegu zilizopandwa na mpunga ulioanza kuota. Wizara ya Kilimo na Maliasili imetoa msaada wa mbegu kwa wakulima walioathirika. Uzinduzi wa utoaji msaada huo ulifanywa na Mhe; Mansoor Jussuf Himid Waziri wa Kilimo na Maliasili mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kati Mhe. Ali Kassim Moh'd, Mkurugenzi wa Idara ya Kilimo ndugu Mberek Rashid, Diwani wa Wadi ya Koani, maafisa wa kilimo na wakulima katika bonde la mpunga la Koani, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja.

Jumuiya ya Wakulima wa bonde hilo walitoa shukrani za dhati kwa kutembelewa na Mhe; Waziri wa Kilimo na Maliasili na kugaiwa mbegu hiyo. katika risala yao walimueleza juu ya athari waliyoipata ya kuharibikiwa na mpunga kutokana na jua kali.

Aidha, wakulima hao waliomba kutengenezewa miundombinu ya umwagiliaji maji kwa hatua za awali za uchimbaji wa kisima, uwekaji wa pampu kwa vile umeme umeshakamilika na waliahidi kuchangia nguvukazi za utengenezaji wa miundombinu ya kujenga matuta kwa ajili ya upitishaji wa maji.

Mara baada ya kukabidhi mbegu hiyo, Mhe; Waziri aliwataka wakulima kuwa na subira juu ya athari iliyowatokea na kuwaahidi kuwa Wizara iko pamoja nao.



Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe; Mansoor Yussuf Himid akimkabidhi mkulima mbegu za mpunga wakati wa uzinduzi wa ugawaji mbegu ya msaada huko Koani, Wilya ya Kati Unguja.

Aidha Mhe Waziri alikubali ombi la kuweka miundombinu ya bonde hilo na alimuagiza Mkurugenzi Idara ya Kilimo kulisimamia agizo hilo ili kuwawekea mazingira mazuri ya uzalishaji wa mpunga

**Hatua zilizochukuliwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kukabiliana na athari za jua kali**

**Mkoa wa Mjini Magharibi**
Wakulima walipatiwa mbegu kilo 825 aina ya BKN SUPA ambazo zilitumika kwa kupanda ekari 33

**Mkoa wa Kasini Unguja**
Baada ya kupata taarifa hiyo Wizara ya Kilimo na Maliasili iliwapatia mbegu wakulima katika Mkoa huo ambapo jumla ya ekari 596 zilipatiwa mbegu kilo 14,605 aina ya BKN SUPA na ekari 35 katika bonde la Koani ziliburugwa tena kwa msaada na kupatiwa mbegu.

**Mkoa wa Kaskazini Unguja**
Wakulima walipatiwa mbegu kilo 9,000 aina ya BKN SUPA na TXD 306 ambazo zilitumika kwa kupanda katika ekari 360



Mbegu ya mpunga ya msaada iliyogaiwa wakati wa uzinduzi huku Koani, Wilya ya Kati Unguja.

# MAANDALIZI YA MALIGHAFI KWA USARIFU

Na Mwanaid Khatib

Malighafi ni mazao, viungo na vifungashio vyenye ubora unaotakiwa kama vile rangi, ukubwa, umbile na kutokuwa na athari za wadudu au maradhi ambavyo vinavyotumika katika utaratibu mzima wa usarifu wa mazao.

Usarifu wa mazao huaanzia katika upatikanaji wa malighafi ambazo zinapatikana kutoka shambani, kununuliwa kutoka kwa wakulima au sokoni. Katika njia zote hizi cha muhimu ni kuzingatia ubora na usalama kwa ajili ya kupata bidhaa bora na kulinda afya za watumiaji wa bidhaa inayozalishwa.

Usarifu ulio bora huanza na uchaguzi wa malighafi iliyo salama kutoka shambani. Ili kuweza kusarifu chakula chenye ubora anatakiwa kuzingatia kanuni bora wakati wote wa usarifu kuanzia upatikanaji wa malighafi. Mazao ghafi yawe yametunzwa vizuri shambani, yamevunwa kwa wakati na yamesafirishwa kwa uangalifu, matunda au mboga za majani yasiwe na michubuko, maziwa, nyama na samaki visiharibike.

Malighafi zihifadhiwe vizuri kabla ya usarifu kuanza. Vyakula vyenye maji maji kama mboga za majani vinahitaji kusarifiwa haraka. Nafaka na mazao yanayofanana yakauke vizuri kabla ya kuhifadhiwa au kusarifiwa.



Wananchi wa kiwa sokoni wakijitafutia bidhaa bora za mazo ya ndizi kwa ajili ya kupata malighafi.

## Upatikanaji wa malighafi

Vigezo vifuatavyo hutumika katika kutambua ubora wa malighafi kutegemea na mazingira yaliyopo; hisia, lishe na chembechembe. Msarifu mdogo azingatie zaidi utambuzi wa hisia maana upo ndani ya uwezo wake. Pia adodose vyanzo vya malighafi hizo ili kuepuka kutumia zilizoathirika na madawa zaidi ya viwango vinavyotakiwa kutoka mashambani. Kwa mwenye uwezo atumie maabara kutambua ubora.

## Usafirishaji wa malighafi

Uangalifu mkubwa unahitajika wakati wa kusafirisha malighafi za vyakula ili viendelee kuwa na ubora hadi wakati wa kusarifu. Msarifu aepuke vichafuzi kama vumbi, takataka na mafuta. Pia malighafi zitunzwe sehemu salama, safi, kavu na isiyo na joto.

## Utayarishaji wa malighafi

Hatua muhimu zinazochukuliwa katika kutayarisha malighafi hutegemea bidhaa na sifa zake kama vile, kupepeta au kusafisha, kuchambua na kuchagua, kuosha, kuweka katika kiwango, kupima kukatakata na kutumbukiza kwenye maji yanayochemka kwa muda mfupi hasa kwa mazao ya mboga mboga na matunda.

Maadalizi pia yazingatie utunzaji wa takataka/makapi ya vyakula, umwagaji wa maji machafu na upimaji sahihi wa uzito. Inatakiwa kutumia maji safi na salama katika kusafisha malighafi na vifaa, maji hayo yawe yamechemshwa, yapoozwe na kuchujwa kwa kitambaa safi kabla ya kutumika. Sabuni ya maji isiyo na harufu ni bora zaidi kwa kuoshea vyombo.



Uangalifu na uwekaji mzuri wa malighafi za mazao ya kilimo kunachangia kupata malighafi zilizobora.



Malighafi iliyovunwa kwa uangalifu na kuhifadhiwa vizuri inasaidia kupata bidhaa nzuri iliyo sarifiwa.

# Matukio ka




Mhe, Balozi Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa pili kushoto akisalimiana na Balozi wa Korea wa kwanza kulia wakiwa pamoja na mwenyeji wao Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid, wapili kulia wakati wa uwekaji wa jiwe la Msingi la Kituo cha mafunzo ya Usarifu wa mazao, Kizimbani.



Makamo wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Hamad, anemimina mpunga katika mashine kwa msimu wa 2011/2012 katika bonde la wakaki alipotembelea maeneo ya kilimo tareh



Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himidi mwenye miwani katikati akiangalia tuta lililojengwa kuzuia maji ya bahari kuingia ndani ya mashamba ya mpunga katika bonde la Usiambini, Mkoani Pembana wananchi kisiwani Pemba.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasi kushoto akimuelezea Makamo wa Pili wa R walizozipata wakulima wa mpunga kutokana kuangalia athari hiyo katika bonde la mpunga


# atika Picha



a Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Seif Sharif ya kupandia, akizindua rasmi kilimo hicho mpunga la cheju, Wilaya ya Kati Unguja e 26/1/2011.




Wizara ya Kilimo na Maliasili Mhe: Mansoor Yussuf Himid kulia akimkabidhi kadi yake ya utambulisho Mwakilishi makaazi wa FAO Tanzania Dk. Louise L. Setshwaelo wakati alipofika Wizarani hapo kujatambulisha rasmi kwa waziri baada ya kuchaguliwa kwake.



li ndugu. Affan Othman Maalim wa mbele ais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi juu ya athari a na kiaangazi wakati alipofanya ziara ya la Kilombero.



Mkuu wa Wilaya ya Kati Mhe. Ali Kassim Moh'd aliyesimama akitoa nasaha zake kwa viongozi na wakulima waliohudhuria uzinduzi wa ugawaji wa mbegu ya msaada ya mpunga iliyotolewa na Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa wakulima wa mpunga walioathirika na kiangazi hapo huko Koani, Wilya ya Kati Unguja.

# WARSHA YA MSWADA WA SHERIA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE KWA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

Na Hashim H. Chande

Warsha ya uhamasishaji wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi juu ya Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe imefanyika tarehe 22/3/2011 katika hoteli ya Ocean View Zanzibar, chini ya uwenyekiti wa Spika wa Baraza la wawakilishi Mhe; Pandu Ameir Kificho.

Warsha hiyo ambayo iliandaliwa na Wizara ya Kilimo na Maliasiali kwa madhumuni ya kuwapa fursa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kujadili rasmu ya Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe nchini kabla ya kuwasilishwa katika kikao cha 23 cha Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuidhinishwa.

Warka wa rasimu hiyo umetayarishwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba nchi yetu inajihakikishia usalama wa chakula na lishe na ina uwezo kutosha wa kukabiliana na upungufu wa chakula na janga la njaa kwa kuweka mikakati na mipango thabiti ya kisera na kisheria.

Warka huo pia una umuhimu mkubwa katika kuangalia nadharia ya uhakika wa chakula na lishe na haki ya binadamu ya kupata chakula wakati wote katika kuendeleza jitihada za Serikali za kupambana na umasikini hapa visiwani na kuharakisha maendeleo ya wananchi kama ilivyofafanuliwa katika MKUZA.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imelipa umuhimu mkumbwa suala hilo hasa katika kuunga mkono fungamano la maridhiano ya kimataifa la Uhakika wa Chakula na Lishe lenye lengo la kuponguza kwa nusu idadi ya watu wenye njaa na viwango duni vya lishe na wasiopata mahitaji yao ifikapo mwaka 2015.

Mapendekezo ya kuanzisha kwa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe ni miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali za kutekeleza Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya mwaka 2008 ambayo imeelekeza kuwepo kwa sheria itakayosimamia uratibu wa uhakika wa chakula na lishe Zanzibar.



Naibu Katibu Mkuu (Kilimo) ndugu Juma Ali Juma akiwasilisha mada katika Warsha ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi

Katika warsha hiyo jumla ya mada tatu ziliwasilishwa ambazo ni:-

1. Dhana ya Uhakika wa Chakula wa chakula na Lishe na haki ya Chakula ambayo iliwasilishwa na Mkurugenzi Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe ndugu Mansura M. Kassim.
2. Uchambuzi wa Hali ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar ambayo iliwasilishwa na Naibu Katibu Mkuu (Kilimo) ndugu Juma A. Juma na
3. Rasimu ya Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe ambayo iliwasilishwa na Mwanasheria ndugu Saleh Mubarak

Dhana ya uhakika wa Chakula na Lishe ni pana kwa vile masuala ya uhakika wa chakula na lishe yametawanyika katika Wizara na taasisi nyengine mbali na Wizara ya kilimo na Maliasili, kwa mfano masuala ya lishe, udhibiti na ukaguzi wa a ubora wa vyakula uko chini ya Wizara ya Afya, masuala ya biashara, kumlinda mlaji na masoko yapo chini ya Wizara ya Biashara, masuala ya udhibiti wa maafa zipo chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, masuala ya ardhi na maji yapo chini ya Wizara ya Ardhi, Maji na Makaazi, madaraka mikoani yapo chini ya Wizara inayoshughulikia Tawala za Mikoa, suala la haki za binadamu yapo chini ya Wizara ya katiba na Sheria, masuala ya Ufugaji na Uvuvi yapo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na masuala ya uzalishaji wa kilimo yapo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Kwa mantiki hiyo mfumo wa utendaji uliopo hivi sasa bado haujatoa uwezo wa kisheria kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili wa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa masuala yote ya Uhakika wa Chakula na Lishe pamoja na kuwa Wizara hii ndiyo iliyopewa agizo na Serikali kusimamia suala hilo, hivyo kupitishwa kwa sheria hii kutaiwezesha Wizara ya Kilimo na Maliasili kusimamia suala hlo kikamilifu.

Katika warsha hiyo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walipata nafasi ya kuupitia na kuuelewa vizuri mswada huo, kuujadili na kutoa michango yao kutokana na mada zilizowasilishwa kwa lengo la kuiwezesha Wizara ya Kilimo kuwa na sheria nzuri na kamilifu ya Uhakika wa Chakula na lishe hapa Zanzibar. Hata hivyo warsha ilitoa umuhimu wa pekee katika kutoa ufafanuzi wa vipengele vilivyomo ndani ya mswada wa sheria hiyo ikiwemo mapendekezo ya muundo wa taasisi ambazo zinapendekezwa kuundwa kisheria kwa lengo la kusimamia na kutoa muongozo juu ya utekelezaji wa maswala ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

# UMUHIMU WA ZAO LA KAROTI

Na Makame M. Abdulrahman

Karoti ni zao linalomea vizuri katika hali ya hewa yenye ubaridi wa wastani, sehemu zenye joto kali haziwezi kumea vizuri na hutoa viazi vyembamba. Zao hili linahitaji udongo mwepesi wa kichanga au tifu tifu na wenye mbolea kiasi. Uzalishaji wake ni wastani wa tani 1,735 kwa mwaka. Hapa Zanzibar zao hili hulimwa katika maeneo ya Bambi, Machui, Kombeni, Dimani na Kizimbani. Hata hivyo, hulimwa na kustawi zaidi katika sehemu zenye baridi kama mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Mbeya na Kagera.

Mizizi ya karoti ndiyo inayotumika kwa chakula na zipo za rangi tofauti zikiwemo nyeusi, pinki, nyekundu na njano. Karoti zenye rangi nyekundu na njano zinasemekana kuwa na virutubisho vingi kuliko karoti nyingine na hulimwa zaidi Tanzania.

**Matumizi ya karoti na faida zake.**

Karoti inaweza kuliwa mbichi, kupikwa na kuchanganywa na mbogamboga, kutengenezwa saladi na juisi. Faida zinazopatikana kutokana na utumiaji wa karoti ni kuongeza vitamini "A" ambayo inatokana na beta-carotene iliyomo ndani ya karoti na pia huongeza vitamini B, C, E na madini ya chuma mwilini.



Hii ni aina ya Karoti inayomea vizuri na kulimwa sana hapa Tanzania

Karoti ina protini kidogo na haina mafuta ukilinganisha na mazao ya jamii ya kunde na yenye asili ya uwanga. Vile vile karoti ina nyuzi nyuzi (fiber) ambazo ni muhimu kwa kukinga kuta za utumbo na kulainisha choo. Karoti inasaidia kuongeza nuru ya macho, kukinga maradhi ya ngozi, magonjwa yenye asili ya kansa na kupunguza tindikali inayodhuru tumboni.

**Kazi za Beta-Carotene na nyuzi nyuzi (fiber)**

Beta-Carotene ni kirutubisho kinachopatikana kwenye karoti ambapo kikiingia mwilini hubadilika na kuwa vitamini "A". Kazi kubwa ya kirutubisho hiki ni kutengeneza retina, kiungo ambacho kipo ndani ya jicho na kuwezesha jicho kuona vizuri hasa kwenye mwanga hafifu. Pia kinasaidia kutengeneza chembecheme kwa ajili ya ngozi, kinywa, macho na viungo vingine laini mwilini. Aidha, beta-carotene hupunguza uwezekano wa mwili kupatwa na magonjwa ya kansa.

Nyuzi nyuzi (Fiber) zinasaidia kulainisha choo, kukinga kuta za utumbo na kupigana na vijidudu tumboni. Ulaji wa karoti unasaidia kuimarisha afya ya mlaji na kukinga maradhi.



Karoti hutumika katika mapishi na vinywaji vya aina tofauti.

# UVUNAJI NA USINDIKAJI WA VANILA

Na Rashid Khamis

Vanilla ni zao la viungo linalotumika kwa mapishi majumbani na viwandani ili kutoa harufu na ladha katika chakula, kastanadi, saladi ya matunda, kahawa, keki na sukari. Spiriti ya vanilla hutumika kwa kutia harufu na ladha katika maziwa ya mgando, mikate, keki, peremende, chokleti, unga wa kastadi na sukari. Ili vanilla yetu ipate soko la nje ya nchi ni lazima iwe na ubora wa hali ya juu na inavutia kwa kuiangalia.



Vanilla iliyokaushwa vizuri na kufanyia gredi ikiwa imefungwa katika vifurushi tayari kwa kuuzwa.

**Uvunaji**

Kwa kawaida podi katika shada la vanilla hupevuka kwa wakati tofauti, hivyo inabidi zivunwe kwa uangalifu moja moja na ni muhimu uvunaji urudiwe mara kwa mara ili kuepuka kuvuna podi changa au zilizopea zaidi. Vanilla zinatakiwa zivunwe zikiwa zimejaa, ngumu, zina rangi ya kijani isiokoza na ncha zake zimegeuka kuwa rangi ya manjano na unjevu unaokaribia asilimia 30.

**Kupasha moto.**

Podi lazima zipashwe moto mara tu baada ya kuvunwa ili kuepusha kupasuka. Maji yapashwe moto hadi kufikia nyuzijoto 65ºC, vanilla zitiwe ndani ya kumuto na kutumbukizwa ndani ya maji ya moto kwa kuninginizwa kwa dakika tatu, tikisha kumuto baada ya sekunde 10 za mwanzo na baada ya kila sekunde 30 ili kuhakikisha podi zote zimepata moto sawa sawa. Nyanyua kumuto na gida maji kwa sekunde 30. wakati wote wa kazi hii joto baridi lazima libaki kati ya nyuzijoto 60 - 63ºC. Ni muhimu kupasha moto kwa muda uliopendekezwa ili kutozuwia kutoka kwa vichocheo vya harufu (vanillin) na kuharibika kwa podi.

**Kuvundisha kwa saa 48**

Baada ya podi kupashwa moto ni lazima kugidwa maji na kutiwa moja kwa moja ndani ya sanduku la kuvundishia na zivundishe kwa kuhifadhiwa katika hali ya joto la 38ºC. Kama ni kidogo basi zizonge ndani ya blanketi na ziwekwe ndani ya sanduku, uondoa hewa ndani ya sanduku na ziache humo kwa muda wa masaa 48.

Sanduku la kuvundishia litengenezwe kwa mbao ngumu liwe na pembe nne, kuta za ndani lazima ziwe fupi kwa sentimita 10 kwa pande zote kuliko kuta za nje. Mwanya baina ya kuta za mbao mbili lazima zijazwe kwa unga wa mbao au makumbi na kushindiliwa vizuri ili kuhifadhi joto lisipotee. Vile vile mfuniko wa sanduku lazima uzibwe vizuri kuzuwia joto lisipotee. Hata hivyo ni vizuri zaidi sanduku kuzongwa blanketi ili kusaidia kuzuwia joto lisipotee na kunyonya maji maji yanayotoka wakati wa kuvundisha. Ikiwa mablanketi hayapatikani basi magunia pia yanaweza kutumika.

Podi zitakuwa tayari zinapabadilika kuwa na rangi ya udongo na kun'gara mafuta. Ikiwa rangi ya kijani bado ipo basi zichemshwe tena kwa sekunde 30 na zirudishwe katika sanduku la kuvundishia kwa muda wa masaa 24 zaidi.

**Kukausha**

Baada ya podi za vanilla kuvundishwa zinaweza kukuashwa kwa kuanikwa juani au kutandazwa katika treya kama ifuatavyo:

**Kuanika juani**

Kwa kupata harufu na ladha nzuri ya vanilla (Vanilin), podi lazima zitolewe katika sanduku la kuvundishia na kuanikwa juani kwa muda wa masaa mawili kila siku kwa muda wa siku 6 -12. Podi zianikwe kwa kutandazwa katika mablanketi au magunia juu ya chanja au majamvi kwa masaa mawili baadae zizongereshwe katika mablanketi au gunia na ziachwe tena juani kwa masaa mawilii mangine. Baadae ziirudishwe ndani ya sanduku na ziachwe humo usiku kucha.

Tahadhari ya kuzikagua podi kila siku na kundo zilizokuwa tayari ni lazima ichukuliwe ili kuepuka kukauka sana. Podi zinakuwa tayari ikiwa ngozi yake imekunjana, laini, zinan'gara mafuta, zinaharufu nzito ya vanillin na zina unyevu kati ya asilimia 55 hadi 60. Kwa kawaida muda wa kuanika unategemea ukubwa wa podi na ubora wake.

**Kukausha ndani ya treya**

Tandaza podi za vanilla katika treya kwa kina cha tabaka moja kwa muda wa wiki tatu zikiwa ni ndogo au hafifu. Wiki sita zikiwa ni kubwa au zina daraja zuri. Treya zitiwe alama ya kuonyesha tarehe ya kuanza ukaushaji pamoja na ubora wa podi, kwa mfano zimepasuka, nzima, hafifu, changa na fupi. Ukaguzi wa podi ufanyike kila wiki kuona kama zimekuwa tayari na zisijezikakauka kupita kiasi. Wakati wa kukausha katika treya hewa ya kutosha inatakiwa ipatikane ili kuepusha podi zisifanye ukungu.

Podi zinakuwa tayari zikiwa bapa na unyevu unakuwa kati ya asilimia 25 – 30, zimegeuka rangi ya kahawia, ngumu kuzikunja kwa vidole, zinapindika bila kukatika lakini bado inaonekana kuwa na mafuta. Hatua ya mwisho ya kushindika ni kuivisha. Hatua hii inahakikisha kuwa vanilla inapata ladha na harufu yake halisi ambapo zinahifadhiwa katika masanduku la mbao au la bati na kufungwa vizuri ili kuepusha upotevu wa unyevu.


# UTUNZAJI BORA WA VIFARANGA VYA KUKU

Na Nassor S. Mohammed

Ufugaji wa kuku ni kazi ambayo inafanywa katika kila nyumba hasa vijijini kwa lengo la kupata nyama na mayai ili kujiongezea kipato na kuimarisha afya za familia. Watu wengi wanafuga kuku lakini hawaelewi kanuni, majukumu na miiko ya ufugaji. Kuku ni lazima watunzwe vizuri ili watoe mazao bora na kufikia lengo lililokusudiwa. Ufugaji huu unaweza kufanywa majumbani pia unatoa uhakika wa kupata kuku wenye sifa nzuri na afya bora.

Vifaranga ni kuku wadogo wa mayai na nyama wanaoanzia siku moja toka kuzaliwa hadi mwezi mmoja. Wafugaji wengi hupata matatizo ya vifo vya vifaranga kutokana na kutokosa kuzingatia huduma muhimu za utunzaji, hivyo tunapaswa kuangalia kwa makini vifaranga vinapototolewa na kuingizwa sehemu za kulelea. Mahitaji ya lazima ya vifaranga ni maji, chakula na hali ya ujoto katika sehemu za kulelea.

**Sehemu ya kulelea**
Vifaranga vinalelewa kwenye mduara kwa muda wa siku 10, inashauriwa kupanua mduara kila baada ya siku tatu. Ondoa mduara siku ya 11 na vifaranga viachwe visambae katika chumba cha kulelea kwa majuma manne,



Vifaranga vinahitaji kupata mwanga wa ili vipate kukiona chakula na vipate joto la kutosha.



Vifaranga lazima vilelewe katika kibanda cha kulelea kilichojengwa vizuri na kupatiwa huduma zote muhimu

baadae vihamishiwe katika banda la kufugia. Vifaa vinavyotumika katika utunzaji wa vifaranga ni vyombo vya kutilia chakula, maji, kandili, seredani au taa za umeme kwa ajili ya kuvipatia joto na mwanga pia hadibodi, boksi kwa kutengenezea mduara, waya wa kuku wa kwa kulizungushia seredani na tandiko la unga wa mbao. Inasisitizwa kuwa vifaa hivyo viwe vimetengenezwa vyema na havivujishi maji wala havimwagi vyakula.

**Angalia:**
Unapotumia makaa hakikisha hayatoi moshi, chumba kina hewa safi na ya kutosha na weka seredani juu ya matofali ili kuzuwia vifaranga wasiliguse na kuungua.

**Kuangalia hali ya ujoto**
Mfugaji anapaswa kuangalia hali ya vifaranga katika mduara uliotengenezwa ili kuelewa hali zao. Ikiwa watajikusanya kwenye chanzo cha joto au kujikusanya sehemu moja ifahamike kuwa joto halitoshi kwa vifaranga hao hivyo inashauriwa aongeze joto.

Iwapo wataonekana kubaki pembezoni mwa mduara, inaonesha joto kali hivyo inabidi lipunguzwe. Joto likiwa kali vifaranga huhema kwa kasi. Hali hii ikiendelea husababisha vifaranga kuanguka, kushindwa kunyanyuka na hatimae hufa.

Inashauriwa kupunguza joto kwa kuvipunguza vifaa vinavyoleta joto na kuwapa maji mengi pamoja na kuwafungulia kwa kuwekewa mwanya mdogo ili watawanyike nje ya mduara ambao utawawezesha kuingia na kutoka.


**Chanjo na kinga kwa vifaranga**
Inasisitizwa vifaranga vipatiwe chanjo na kinga dhidi ya maradhi ikiwemo Gumboro, Mahepe, Mafua na magonjwa ya kuharisha kwa mpagilio maalum kutegemeana na matumizi ya vifaranga husika.

# UDHIBITI WA WADUDU WAHARIBIFU WA MINAZI

Na Neema A. Khalfan

Wadudu waharibifu wa minazi wapo aina nyingi lakini walio muhimu na wanaoleta madhara katika visiwa vyetu vya Zanzibar ni bungu wa minazi, chonga, mchwa na utitiri.

**1. Bungu wa minazi**



Bungu wa minazi ni mdudu wa asili hapa Afrika Mashariki.

**Athari za bungu**

Bungu wa minazi ni mdudu ambae hufyonza vidaka na vidaka vilivyoshambuliwa hupata vidonda na huanguka na hutaga mayai katika makuti na makole na pia bungu aliyepevuka anao uwezo wa kuruka kutoka mnazi mmoja hadi mwengine.

**Madhara yake**

Madhara ya bungu yanayotokana na mate yake yanasababisha vidonda kwenye vidaka na hufanya makovu na hutoa gundi na vidaka vyengine vinaweza kuhimili mashambulizi lakini nazi zake huwa ndogo na hazifai kwa mbegu.

**Kudhibiti bungu kwa kutumia majimoto**

Njia za kudhibiti bungu kwa kutumia wadudu wa majimoto, wadudu hawa hufukuza na kuuwa bungu na hupatikana kwa kupanda miti ya aina ya mistafeli, mikarafuu, mipea, mifenesi, miti ya aina ya michungwa, mipera na miti mengine inayopendwa na majimoto.

Mafanikio ya kuzuia bungu kwa kutumia maji moto yanaambatana nakutokuwepo kwa sisimizi na sangara shambani, na sisimizi wanaweza kudhibitiwa kwa kutumia dawa Amdro.

**Kudhibiti bungu kwa kutumia dawa**

Njia nyengine inyoweza kutumika katika kudhibiti bungu ni kwa kutumia madawa. Hata hivyo njia hii inaweza kutumika wakati minazi bado mifupi na pia ni ghali na huhitaji uangalifu mkubwa.

**2. Chonga**



**Athari za chonga**

Chonga aliepevuka hutoboa mpaka kwenye kitale cha mnazi, hivyo huharibu makuti machanga kabla ya kuchanua. Makuti yaliyoshambuliwa yanapochanua huonyesha alama ya "V". Chonga akila kitale chote, mnazi hufa. Hii inatokea mara nyingi kwenye minazi michanga ya umri chini ya miaka minne.

**Kuzuia chonga**

Chonga anaweza kudhibitiwa kwa njia kuu mbili.

**Kuharibu makazi ya chonga.**

Njia hii hutumika ili kuzuia chonga wasiendelee kuzaliana. Magogo ya minazi iliyokufa yaangushwe na yatumiwe.

**Kuwaondoa chonga kwa ndoana (Hook)**

Ndoana iingizwe kwenye shimo ambalo chonga anakula; kisha atolewe na kuuliwa.

**3. Mchwa**



Mchwa ni wadudu wanaoshambulia sana minazi na hasa ile michanga michanga ambayo ni dhaifu na miche ambayo bado iko kitaluni au mara tu baada ya kupandikizwa shmbani. Mchwa huishi kwenye vichunguu ardhini na hutengeza njia kwa kutumia udongo kutoka kwenye vichunguu hadi kwenye mazao wanayoyashambulia. Wadudu hawa hukata na kula karibu sehemu zote za minazi michanga kama vile shina, makuti na hata mbegu yenyewe. Mashambulizi ya mchwa yanatokea sana wakati wa kiangazi.

**Kumzuia mchwa**

Mchwa wanaweza kuzuiwa kwa kustawisha miche kwenye vifuko maalum vya nailoni (polybag) katika kitalu, kutumia majivu ya mapumba ya mpunga, miti aina ya aufobia (Eurphobia). Njia nyengine ni ile ya kutumia dawa ya aina ya Marshaal suScon.


Ni bora kuanziasha kitalu sehemu ambayo haina mchwa.

**4. Utitiri**

Utitiri ni wadudu wadogo ambao huoneka na vyema kwa kutumia darubini. Wadudu hawa hushambulia sehemu ya juu ya kidaka ambayo imefunikwa na maganda

Ahari zaidi hutokea kenwe vidaka vyenye miezi mitatu hadi sita ambayo vinaweza kuanguka na zaidi wakati wa kiangazi. Nazi zilizoshambuliwa hupata mikwaruzo na mara nyingi ganda lake hupasuka. Hakuna njia inayoaminika ya kuzuia wadudu hawa.

Ili kupata mazao bora, mengi na yenye usalama kwa afya fuata maelekezo ya mabwana shamba na waone wafanyakazi wa Kitengo cha minazi na kituo kilichopo karibu yako.



# UVUNAJI WA MAJI YA MVUA

Na Amour U. Vuai

Mvua ina umuhimu mkubwa katika uhai wa viumbe, miaka ya hivi karibuni visiwa vyetu vimekabilwa na uhaba wa mvua kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, miongo na tabia nchi ulimwenguni. Tafiti zinaonyesha kwamba maji mengi ya mvua hupotea na kuishia baharini bila ya kutumiwa na inakisiwa maji yanayopotelea baharini ni mita za ujazo 881.3 milioni sawa na asilimia 24 kwa Unguja na mita za ujazo 797.4 milioni sawa na asilimia 53.3 kwa Pemba. Hali hii inasababisha kupungua kwa maji katika vyanzo vyake, ambapo kumepelekea uhaba kwa matumizi ya kilimo, mifugo na majumbani.Hivyo, hatunabudi kuvuna maji ya mvua na kuyatumia ipasavyo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wenye tija.



Bwawa lililojengwa kwa ajili ya kukusanya maji ya mvua ili kuyatumia kwa kazi za kijamii kama kilimo na uvuvi.

**Uvunaji wa maji ya mvua**

Uvunaji wa maji ya mvua ni teknolojia inayotumika kuyakusanya na kuyahifadhi kwa matumizi, kabla ya kupotea hewani na ardhini. Hii ni mbinu rahisi na yenye gharama ndogo ambayo inakusanya, inasambaza na inahifadhi maji ya mvua kutoka kwenye mapaa ya nyumba na ardhini kwa matumizi ya majumbani, kwa mifugo, kumwagilia mashambani, viwandani na kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira. Maji ya mvua yaliyokusanywa kutoka katika mapaa ya nyumba, yanaweza kutoa mchango muhimu wa upatikanaji wa maji ya kunywa, maji haya ni mazuri na wala hayahitaji kutiwa dawa kabla ya matumizi ingawa, baadhi ya mapaa hukusanya maji ya mvua ambayo ni hatari kwa afya ya binadamu hivyo, maji hayo hutumika kwa kusafishia vyoo, kufulia nguo, kumwagilia bustani na kuoshea magari.

**Aina za uvunaji wa maji ya mvua**

**1. Uvunaji wa mvua kutoka juu ya paa la nyumba.**
Hii inafanyika kwa kuwepo eneo la paa la nyumba, mikingo ya kusafirishia maji na tangi la kuhifadhia maji. Wingi wa maji yanayovunwa utategemea ukubwa wa paa na mvua ambayo inapatikana katika sehemu husika.

**2. Uvunaji wa maji mashambani** kwa mfano mradi wa jamii (PADEP) wa ukulima wa mpunga uliopo Kiboje Mkwajuni. Uvunaji wa aina hii unatakiwa kutayarisha vishamba vyenye pembe nne ambalo ukubwa wake unatakiwa kuwa na urefu wa kwenda juu usiopungua mita 0.75 na baada ya kushindilia vizuri ubakie mita 0.5. Hivyo, eka moja inagawanywa katika vishamba vinne (4) vilivyo sawa vilivyojengwa kwa matuta, kila kimoja kitakuwa na urefu wa mita 50 na upana mita 20 ambacho kitakuwa na ukubwa wa mita za mraba 1000 ukubwa huo unatosha kwa mkulima mmoja na kuvuna maji ya mvua. Mvua zinaponyesha maji huingia moja kwa moja ndani ya kishamba. Wastani wa mavuno ya mpunga ni polo nane katika kishamba hicho zenye ujazo wa kilo 50 kwa kila moja.

**NAMNA YA KUTAYARISHA KISHAMBA**
Hatua muhimu zinazopendekezwa wakati wa utayarishaji wa kishamba cha mpunga kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua
Kuweka sawa kishamba ni muhimu na hufanyika kama ifuatavyo:-
Kuondoa vilima ndani ya kishamba kwa kutumia bao ambalo linaitwa fatuma au bero na kuutawanya udongo sehemu ambazo zipo chini, kazi hii hufanyika mara tu baada ya kuburuga, unatakiwa kuhakikisha kwamba wakati wa kuchimba sehemu ya udongo wa juu uweke pembeni na baadae uurudishe ili usijekuhamisha, udongo wenye rutuba na ule wa chini ndio unaweza kuuhamisha na kuuweka kwenye matuta.

Changanya udongo ili ubakie kwenye rutuba ya asili, hakikisha unaangalia muinamo ili upingane nao na ni muhimu kuweka misingi ya maji yaliyozidi ili kupunguza mafuriko pindi tu yanapotokea.

**3 Uvunaji wa maji ya mvua yenye kutembea ardhini**
Aina hii ya uvunaji maji hutokea mara tu mvua inaponyesha ardhini na huanza kufikia kwenye mafikio yake, hatimae hutiririka na kufikia kwenye hifadhi kama vile madimbwi. Maji haya baadae yanaweza kutumika kwa kumwagilia mazao ukiwemo mpunga.
Teknolojia ya uvunaji wa maji hapa Zanzibar si ngeni isipokuwa isipokuwa bado haijaipa msukumo unaostahiki, pamoja na juhudi zilizochukuliwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili kuanzisha miradi ya uvunaji wa maji ya mvua inaonekana kuwa bado wananchi wengi hawajafaidika. Wizara ya Kilimo inawataka viongozi katika ngazi zote nchini kuhamasisha wananchi kuhusu matumizi ya teknolojia hiyo ili kupunguza tatizo la maji linalojitokeza katika nchi. Uvunaji wa maji ya mvua utawawezesha wananchi kupata maji ya uhakika ambayo yatahifadhiwa kwa matumizi ya baadaye badala ya kuyaacha maji hayo kuishia ardhini.

# Jarida la KILIMO

Toleo la Tano
Januari - Machi, 2011


# MRADI WA KUKUZA MASHIRIKIANO

Na Asya Filfil

Kamisheni ya bahari ya hindi imezindua mradi wa kukuza ushirikiano katika kilimo tarehe 8 December 2010 ambao unaitwa Mradi wa Uwiano wa Kimaumbile "Agroecology". Kufuatia mpango wa kanda wa uhifadhi wa mimea uliotekelezwa mwaka 2003 hadi 2008; Mradi huu mpya unalenga katika ukuaji wa kilimo na mazingira yake katika visiwa vya Bahari ya Hindi (France Re union, Comoro, Madagaska, Mauritius na Seyshelles) na Zanzibar. Mbinu zitakazotumika katika mradi huu zitazingatia mazingira, bioanuai na wakati huo huo kuongeza mavuno. Mbinu hizi zitazingatia elimu ya maumbile ili kupunguza matumizi ya pembejeo za kemikali, maji na mabaki ya nishati katika kilimo. Miradi imepangwa kuchunguza pembejeo kwa kuzingatia tathmini ya carbon na kuweka mkazo kwenye kazi zake halkadhalika kuzingatia mabadiliko ya hali ya hewa na matumizi ya pembejeo hizo kwa wakulima.

Mradi huu unatekelezwa na kamisheni ya visiwa vya bahari ya hindi na unatarajiwa kufanyakazi katika mtandao wa watendaji ulioshiriki katika awamu ya uzinduzi ikiwemo 1) miradi ya kilimo inayofadhiliwa na IFAD, pamoja na mashirika mengine ya maendeleo, huduma za elimu kwa wakulima kitaifa, vituo vya utafiti, asasi zisizo za kiserikali, vituo vya mafunzo ya kilimo na taasisi binafsi, mtandao pia uko wazi kwa mashirika yenye dhamira ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mradi wa agroecology unadhaminiwa na mfuko kimataifa wa maendeleo ya kilimo (IFAD), shirika ambalo linafadhili miradi ya maendeleo ya kilimo katika visiwa vya Madagaska, Comoro, Mauritius na Zanzibar, na kuwepo kwa Ufaransa kupitia mradi wa elimu kwa wakulima na mtandao endelevu wa uhifadhi wa mimea unaodhaminiwa na umoja wa maendeleo wa Ulaya katika serikali ya Ufaransa kwenye visiwa vya Re union.

Kamati ya Uongozi ya mradi katika kila nchi za visiwa vya Bahari ya Hindi itakuwa na wawakilisha (NFP) wawili kutoka Taasisi za Serikali na mwengine kutoka Asasi za Kiraia, pamoja na mwakilishi kutoka katika taasisi na miradi inayojishughulisha na Agroecology.



Wajumbe wa kamati ya uongozi wakati wa kikao cha uzinduzi wa mradi Mauitius

Kila nchi imekubali kuanzisha jukwaa na kuandaa mkutano utakaojadili muelekeo wa mafanikio yaliyopatikana kwenye agroecology na mpango wa utekelezaji wa mradi katika kipindi cha mwanzo 2011. Madagaska ilitoa muelekeo wao wa vipando vya kuhifadhi ardhi, uliowasilishwa na mwakilishi wa kikundi cha Madagaska katika mkutano wa uzinduzi.

Kazi zilizoainishwa katika mtandao wa agroecology ni:

- Uanzishwaji wa mtandao
- Uanzishwaji wa jukwaa litakalowajibika na maendeleo ya agroecology ya kila nchi
- Kubadilishana matembezi baina ya wakulima na wataalamu katika visiwa
- Kubadilishana utaalamu
- Utekelezaji wa kumbukumbu za kudumu (permanent reference table)
- Kuanzisha maeneo ya utaalamu (pole of competence)
- Kuimarisha taarifa za mtandao.

Mfumo wa ushirikiano wa kanda umeanzishwa kukidhi mahitaji ya mradi huo. Aidha, kutakuwa na mtandao wa internet ili kurahisisha taarifa za watendaji wa nyanja ya kilimo na kukusanya taarifa za viumbe waharibifu na wenye faida katika kilimo na kuchukua hatua tofautikuhusiana na uhifadhi , agroecology and uendelezaji wa PRPV.

Kati ya hatua zilizoainishwa na France reunion ni:

- Kuzisaidia nchi kukuza uwezo wa kuainisha maradhi ya wadudu na kukuza uwezo wa kupambana na spp zenye kuleta uharibifu.
- Kubadilishana uwezo juu ya matukizi ya mbolea za asili – mboji.
- Kufanya majaribio kusaidia homologation ya pembejeo ambazo hazina dhara kwa mazingira.
- Kuwapa mafunzo wataalamu na wakulima juu ya mbinu mbali mbali za kilimo, kilimo hai na kubadilishana baina ya wakulima wa visiwa vya bahari ya hindi.

Hatua hizi zitashirikisha wadau mbali mbali wakiwemo CIRAD (Center for International Research and Agriculture Development), serikali ya Ufaransa na mashika mengine ya maendeleo yaliyoshiriki katika warsha hii ya uzinduzi.


GAZETI HILI HUTOLEWA KILA BAADA YA MIEZI MITATU NA
WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI - ZANZIBAR
P. O. Box 159 Zanzibar, Simu: +255 24 2230986, Fax: +255 24 2234650
Barua pepe: kilimo@zanlink.com, Tovuti: www.kilimoznz.or.tz